Majibu yaliyopendekezwa:

1. Mwanafunzi ataje aina yoyote ya michezo kama vile: kandanda, riadha, mpira wa pete, kuruka kamba na kadhalika.

2. Sababu zinazomfanya kuupenda mchezo aliochagua/aliotaja. Kwa mfano :
   i. Ni rahisi kuucheza.
   ii. Marafiki wanaupenda pia.
   iii. Si rahisi kuumia unapoucheza.
   iv. Ni mchezo wa kusisimua.
   v. Ni mchezo wa kitamaduni.
   vi. Vifaa vya kuucheza vinapatikana kwa urahisi.

3. Ushauri kwa rafiki kushiriki michezo:
   i. Kumweleza kuwa michezo ni muhimu kwa afya.
   ii. Michezo huondoa uchovu.
   iii. Michezo hukuza urafiki.
   iv. Huimarisha mahusiano.
   v. Ni njia nzuri ya kutumia muda wa ziada.
   vi. Huimarisha umakinifu wa mwanafunzi darasani.
   vii. Michezo inaweza kukuza ubunifu.
   viii. Michezo inaweza kuwa kitega uchumi.